## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI OKTOBA, 2021 NA MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2021.

**Dondoo za tathmini ya Oktoba, 2021 na mwelekeo wa Novemba, 2021:**

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Oktoba, 2021 na kutoa mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Novemba, 2021 nchini.

- Katika kipindi cha mwezi Oktoba, baadhi ya maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo machache ya magharibi mwa nchi yalipata vipindi vya mvua. Aidha, maeneo machache ya ukanda wa pwani yalipata vipindi vichache vya mvua.
- Katika mwezi Novemba, 2021 mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Magharibi, kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini, pwani ya kusini na kusini mwa mkoa wa Morogoro). Hali ya joto inatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA, 2021.

Katika kipindi cha mwezi Oktoba,2021 baadhi ya maeneo ya Ukanda wa Ziwa Victoria na maeneo machache ya magharibi mwa nchi yalipata vipindi vya mvua. Aidha, maeneo machache ya ukanda wa pwani yalipata vipindi vya mvua. Kiwango cha juu cha mvua cha milimita 48.0 za mvua kiliripotiwa katika kituo cha Iringa mnamo tarehe 31 Oktoba, 2021, ikifuatiwa na kituo cha Matangatuani kilichopo Pemba kilichopima milimita 45.6 mnamo tarehe 19 Oktoba, 2021 na kituo cha Mwanza kilichopima milimita 33.4 mnamo tarehe 14 Oktoba, 2021. Kwa upande mwingine, hali ya joto iliendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususan ukanda wa pwani.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**
*727B –00/2019*

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI NOVEMBA, 2021

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la kitropiki ya bahari ya Pasifiki linatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani. Joto la bahari la wastani linatarajiwa katika maeneo ya upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi wakati upande wa mashariki mwa Bahari ya Hindi unatarajiwa kuwa na joto la bahari la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kupunguza upepo wenye unyevunyevu unaovuma kuelekea maeneo ya pwani. Hali ya joto la wastani hadi chini kidogo ya wastani inatarajiwa eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki karibu na pwani ya Angola. Hali hii inatarajiwa kuwa na mchango hafifu wa upepo wenye unyevunyevu kuvuma kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

### 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI NOVEMBA, 2021

Kwa ujumla vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, na ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021. Aidha, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika mwezi Novemba, 2021. Kwa upande mwingine, vipindi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini kutokana na upungufu wa mvua unaotarajiwa. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki ya kwanza na ya pili. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache katika mwezi Novemba, 2021. Aidha, ongezeko kidogo la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria. Hata hivyo, upungufu wa mvua unatarajiwa katika wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2021.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea. Hata hivyo, vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**
***727B –00/2019***

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika wiki ya pili ya mwezi Novemba,2021 katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Novemba, 2021.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, mvua za Msimu zinatarajiwa kuanza katika wiki ya tatu ya mwezi Novemba, 2021. Ongezeko kidogo linatarajiwa katika wiki ya nne ya mwezi Novemba.

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI DISEMBA, 2021.

Katika kipindi cha mwezi Disemba, 2021 vipindi vya mvua vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, hali ya joto inatarajiwa kuwa ya kawaida hadi juu ya kawaida katika baadhi ya maeneo nchini.

## 2.4 USHAURI

Vipindi vichache vya mvua vinavyotarajiwa vinaweza kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika ardhi. Wakulima pamoja na jamii kwa ujumla wanashauriwa kupata na kufuata ushauri wa maafisa ugani juu ya matumizi sahihi ya mvua hizo.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Novemba, 2021 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Ubungo Plaza, Ghorofa ya 3, 388 Morogoro Rd
S.L.P. 3056, 16102 Dar es Salaam, Tanzania. Nukushi: +255 22 2460735, Simu: +255 22 2460706-8
Barua pepe: met@meteo.go.tz, Tovuti: www.meteo.go.tz